GOVERNMENT NOTICE NO. 139 published on 22/04/2016

THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT ACT

(CAP.191)

# GUIDELINES

*(Made under Section 13(3))*

THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT (DESIGNATION OF NATIONAL CLEANLINESS DAY) GUIDELINES, 2016

WHEREAS, section 13(1) of the Environmental Management Act empowers the Minister responsible for environment to issue guidelines necessary for the promotion, protection and sustainability of the environment;

AND WHEREAS, sections 13(2) and (3) further empowers the Minister to designate a specified time and give directives relating to performance of activities at such designated time;

NOW THEREFORE, in exercise of the powers confered on the Minister by section 13 of the Environmental Management Act, I do hereby declare as follows-

Citation

1. These guidelines may be cited as the Environmental Management (Designation of National Cleanliness Day) Guidelines, 2016.

Designation of National Cleanliness Day

2. Every Saturday of the last week of each month is hereby designated as a National Cleanliness Day.

Designated activities

3. All Sector Ministries, Government Departments, the National Environment Management Council, National Environmental Advisory Committee, City, Municipal or District Environmental Management Committee, Agency or any other public or private institution are, for each day designated in terms of regulation 2, hereby empowered to-

(a) supervise and coordinate the activities specified in the Schedule; and

(b) coordinate the implementation of the specified activities in the manner provided for in the Schedule.

Punishment

4. The provision of the Environmental Management Act, Environmental Management (Solid Waste Management) Regulations, 2009 and respective by- laws of local government authorities shall have effect to penalties which may be imposed against the non-compliance of the directive of the Minister and directives of entities specified under regulation 3.

## SCHEDULE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA USAFI WA MAZINGIRA KILA SIKU YA JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI

**YALIYOMO**

**1. UTANGULIZI……...…………………………….……..…..................................………. 4**

**2. LENGO LA KURASIMISHA KILA JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI KUWA SIKU YA USAFI KITAIFA ......................................................................................................4**

**2.1** Umuhimu wa Usafi wa Mazingira kila Siku ya Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi ................**4**

**2.2.** Madhara (Magonjwa) Yatokanayo na Uchafu wa Mazingira………………………..…… **5**

**2.3.** Muda wa Usafi kila Siku ya Jumamosi ya kila Mwisho wa Mwezi ……………………....**5**

**3. LENGO LA MWONGOZO…………………..…...……….....…...........................................…..5**

**4. SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA .........................................................................................5**

**5. HATUA ZA UTEKELEZAJI ...................................................................................................6**

**5.1.** Kazi zitakazofanywa na wanachi..............................................................................................6

**5.2.** Kamati ya Utekelezaji na Majukumu yake..............................................................................**6**

**5.3.** Majukumu ya Kamati **......................................................................................................6**

**6. UFUATILIAJI NA TATHIMINI YA SHUGHULI ZA USAFI WA MAZINGIRA**

**6.1.** Ufuatiliaji………..…......…………………….........................................……………….......**7**

**6.2.** Tathmini…………......………………………….......................................……………...**7**

**6.3.** Utaratibu wa Ufuatiliaji na Tathmini ......................................................................................**8**

**6.3.1.** Ngazi ya Mtaa/Kitongoji/Kijiji .............................................................................................. **8**

**6.3.2**. Ngazi ya Kata ………………………………………………………………………..…….**8**

**6.3.3.** Ngazi ya Halmashauri ya Mji, Wilaya, Manispaa na Jiji …………………………..……..**9**

**7. ADHABU KWA AMBAYE HATAFANYA USAFI** .................................................................**9**

**8.** Fomu ya ufuatiliaji wa usafi wa mazingira....................................................................................**10**

**1. UTANGULIZI**

Ofisi ya Makamu wa Rais ina jukumu la kusimamia Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira nchini. Katika kuhakikisha Mazingira yanatunzwa vizuri, Ofisi inasimamia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, na imeandaa Kanuni na Miongozo mbalimbali inayolenga kusimamia shughuli hizo. Ili kuhakikisha Mazingira yanatunzwa, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Kanuni zake zimezipa pia mamlaka Serikali za Mitaa kusimamia Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira katika maeneo yao husika.

Hata hivyo, licha ya jitihada zinazofanywa na Serikali, bado kuna changamoto nyingi zinazoathiri Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira, ikiwamo taka zinazotokana na shughuli za kibinadamu katika maeneo ya makazi na maeneo ya shughuli za kiuchumi.

Kanuni za Udhibiti wa Taka Ngumu za Mwaka 2009 zinatamka kuwa, kila raia anayeishi Tanzania na Serikali za Mitaa zitahakikisha kuwa usafi wa mazingira unafanyika na mazingira yanatunzwa.

Ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli hii kwa ufanisi, Ofisi imeandaa Mwongozo huu unaoelekeza taratibu na namna bora ya kutekeleza Tamko la Serikali la Kuitangaza kila Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi kuwa Siku ya Usafi wa Mazingira Kitaifa.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Aidha, Mwongozo huu ulijadiliwa na wadau mbalimbali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Mwongozo huu umeandaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 13 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 pamoja na Kanuni ya 8 ya Kanuni za Udhibiti wa Taka Ngumu za Mwaka 2009 na hivyo kuzipa nguvu ya kisheria Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia utekelezaji wake.

**2. LENGO LA KURASIMISHA KILA JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI KUWA SIKU YA USAFI KITAIFA**

Ili kutunza na kuhifadhi Mazingira, Serikali imeamua kutangaza kila Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi kuwa Siku ya Usafi wa Mazingira Kitaifa na kuirasimisha. Aidha, lengo la kurasimisha siku hii ni kuwa na jitihada za pamoja kama Taifa za kuwashirikisha wananchi moja kwa moja katika kufanya usafi wa mazingira na kuondoa takataka zote zinazozalishwa katika makazi yao na maeneo wanayofanyia shughuli za kiuchumi angalau mara moja kwa mwezi.

Ifahamike kwamba siku nyingine tofauti na siku hii, Halmashauri za Miji na Manispaa zitaendelea na utaratibu wa kawaida wa siku zote wa kufanya usafi na kuondoa taka kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazohusu Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira.

**2.1. Umuhimu wa Usafi wa Mazingira kila Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi ni:**

a) kudhibiti na kuzuia kuenea kwa magonjwa yanayosababishwa na uchafu wa mazingira kama vile kipindupindu, malaria, n.k.;
b) kuwa na mazingira mazuri yanayopendeza kiafya na kijamii;
c) kupunguza magonjwa ya mlipuko; na
d) kutoa hamasa kwa wananchi kutunza mazingira kila wakati.

**2.2. Madhara (Magonjwa) Yatokanayo na Uchafu wa Mazingira**

Ifuatayo ni orodha ya baadhi ya magonjwa yanayosababishwa kwa namna moja au nyingine na uchafu wa mazingira. Magonjwa hayo ni:

a) Kipindupindu;
b) Homa ya matumbo *(typhoid)*;
c) Kuhara/kuhara damu *(amoeba);*
d) Minyoo/funza;
e) Malaria;
f) Polio;
g) Uti wa mgongo;
h) Kifua kikuu (TB);
i) Ugonjwa wa macho *(trachoma)*; na
j) Kichocho.

**2.3. Muda wa Usafi wa Mazingira kila Siku ya Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi**

Usafi wa mazingira kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi utafanyika kuanzia **saa 12:00 asubuhi hadi saa 3:00 asubuhi**. Katika muda huo, shughuli nyingine zote za kiuchumi au biashara zitasitishwa.

**3. LENGO LA MWONGOZO**

Lengo la Mwongozo huu ni kuhakikisha kuwa kunakuwa na utaratibu na mbinu zinazofanana katika utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli za usafi wa mazingira kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi katika maeneo ya mitaa, vitongoji, vijiji, Halmashauri za miji, manispaa na majiji ili kuleta ufanisi unaotakiwa.

**4. SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA**

Kazi zifuatazo zitafanyika:

(a) uhamasishaji wa usafi wa mazingira kuanzia ngazi ya makazi, maeneo ya shughuli za kiuchumi hadi maeneo ya umma;
(b) kila mwananchi na mamlaka husika kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya makazi, maeneo ya shughuli za kiuchumi na maeneo ya umma na kuondoa taka hizo;
(c) kuandaa sehemu za kukusanyia taka na kuziondoa, kuziteketeza au kuzipeleka zinakotumika tena kama malighafi kwa utaratibu unaokubalika;
(d) kuandaa na kukusanya takwimu za usafi wa mazingira;
(e) kuandaa orodha ya raia ama kaya ambazo hazikufanya usafi wa mazingira;
(f) kuandaa orodha ya maeneo ambayo hayakufanyiwa usafi;
(g) ufuatiliaji na tathmini;
(h) kuelimisha jamii kuhusu mahusiano baina ya usafi wa mazingira na ugonjwa wa kipindupindu pamoja na magonjwa mengine na namna ya kupambana nayo au kuyazuia;
(i) uundaji wa vikundi vya usafi wa mazingira kwenye mitaa au vitongoji; na
(j) kuainisha mahitaji ya usafi wa mazingira na changamoto zake.

**5. HATUA ZA UTEKELEZAJI**

Katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli zilizotajwa hapo juu katika Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji pamoja na mitaa, vitongoji na vijiji mambo yafuatayo yatafanyika:

**5.1. Kazi Zitakazofanywa na Wananchi**

Kila mwananchi atafanya usafi wa mazingira kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi katika maeneo ya makazi, maeneo ya shughuli za kiuchumi na maeneo ya umma. Izingatiwe kwamba usafi wa mazingira siku hiyo katika maeneo ya shughuli za kiuchumi utafanywa kwanza na wafanyabiashara wa maeneo husika isipokuwa itakapokuwa imeamriwa vinginevyo na Kamati ya Utekelezaji. Aidha, kazi zitakazofanyika siku hiyo ni pamoja na:

(a) kufyeka nyasi, majani na vichaka katika maeneo ya makazi yao, maeneo ya shughuli za kiuchumi na umma yanayowazunguka kama vile barabara, njia, genge, soko, n.k.;
(b) kufagia nyumba na maeneo ya makazi yao, maeneo ya shughuli za kiuchumi na umma yanayowazunguka kama vile barabara, njia, genge, soko, n.k.;
(c) kukusanya taka zote na kuzipeleka katika maeneo yaliyoainishwa na Kamati ya Utekelezaji kwa ajili ya kuteketezwa au kuondolewa;
(d) kuondoa taka na kupeleka mahali sahihi na kuzitupa; na
(e) kuteketeza taka zote ambazo si lazima ziondolewe kwa utaratibu ulioainishwa na Kamati ya Utekelezaji.

**5.2. Kamati ya Utekelezaji na Majukumu yake**

Kila Serikali ya Mtaa itaunda Kamati ya Utekelezaji wa Usafi wa Mazingira Siku ya Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi itakayojulikana kama Kamati ya Utekelezaji. Kamati ya utekelezaji itakuwa na wajumbe kumi ambao kati yao wanawake hawatapungua watatu na hawatazidi watano.

Kamati ya Utekelezaji itakuwa madarakani kwa kipindi cha mwaka mmoja kabla ya kuteua au kuchaguliwa wajumbe wengine. Kamati hiyo itafanya kazi chini ya Kamati inayoshughulika na masuala ya mazingira katika ngazi ya Serikali ya Mtaa, Kitongoji au Kijiji kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake. Na kwa sababu hiyo Wajumbe wa Kamati hizo hawatakuwa Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji.

**5.3. Majukumu ya Kamati**

Pamoja na majukumu mengine, Kamati itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kufanya usafi na kusimamia usafi wa mazingira;
(b) kuandaa sehemu za kukusanyia taka na kusimamia utaratibu wa kuziondoa au kuziteketeza;
(c) kuandaa na kukusanya takwimu za usafi wa mazingira;
(d) kuandaa orodha ya raia au familia ambayo haikufanya usafi wa mazingira;
(e) kuandaa orodha ya maeneo ambayo hayakufanyiwa usafi;
(f) kufuatilia na kuandaa tathmini ya usafi wa mazingira na kuiwasilisha kwa Kamati ya Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira ambayo nayo itaiwasilisha Serikali Kuu;

(g) kuainisha mahitaji ya usafi wa mazingira na changamoto zake na kuwasilisha katika Kamati ya Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira kwa ajili ya utatuzi;
(h) kuhamasisha jamii kufanya usafi wa mazingira; na
(i) kufanya kazi yeyote inayohusiana na usafi wa mazingira siku ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi.

## 6. UFUATILIAJI NA TATHMINI YA SHUGHULI ZA USAFI WA MAZINGIRA

Lengo la kufanya zoezi la ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za usafi wa mazingira kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi ni kufahamu iwapo Tamko la Serikali linatekelezwa na shughuli zilizopangwa zinafanyika na zinaleta matunda yaliyokusudiwa. Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini yanahitajika kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa shughuli za usafi wa mazingira kwa kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi pamoja na kuchukua hatua zaidi za utekelezaji wa siku hiyo. Aidha, ufuatiliaji wa karibu utafanyika mara kwa mara ili kupata taarifa na takwimu sahihi zitakazotoa picha halisi kuhusu utekelezaji wa Tamko la Serikali na shughuli zilizopangwa.

### 6.1 Ufuatiliaji

Mambo muhimu ya kufuatilia katika utekelezaji wa shughuli za usafi wa mazingira siku ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi kwenye mitaa, vitongoji na vijijini ni pamoja na kuthibitisha kuwa:

(a) usafi unafanyika kama ilivyopangwa;
(b) takataka zinaondolewa au kuteketezwa kama ilivyopangwa;
(c) shughuli zinazotekelezwa zinaashiria kutoa matunda; na
(d) maeneo ambayo hayakufanyiwa usafi yanafahamika hasa kama maeneo hayo hayajafanyiwa usafi zaidi ya mara mbili; na fidia inalipwa na mtu ama kaya ambayo haikufanya usafi.

### 6.2 Tathmini

Tathmini itafanyika ili kuona kama utekelezaji wa shughuli za usafi wa mazingira siku ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi inafikia lengo lililotarajiwa, Tathmini itafanyika kila robo mwaka, nusu mwaka na mwisho wa mwaka.

.
Masuala yatakayofuatiliwa wakati wa tathmini ni pamoja na:-

a) idadi ya mitaa/vijiji vilivyofanyiwa usafii na ambavyo havikufanyiwa usafi;
b) idadi ya maeneo ya umma na shughuli za kiuchumi ambayo hayakufanyiwa usafi;
c) idadi ya kaya ambazo hazikufanya usafi;
d) hali ya usafi siku ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi ilivyo kitaifa/nchi nzima; na
e) changamoto za usafi kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi na utatuzi wake.

### 6.3 Utaratibu wa Ufuatiliaji na Tathmini katika Ngazi Mbalimbali

#### 6.3.1. Ngazi ya Mtaa/Kitongoji/Kijiji

Timu ya ufuatiliaji itatoka miongoni mwa Kamati ya Utekelezajii. Wajumbe wa timu hii hawatazidi watu sita wakiwemo wanawake. Timu itafanya shughuli za ufuatiliaji mara baada ya usafi siku ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi au siku inayofuata. Timu hii itatembelea na kukagua

utekelezaji wa masuala ya usafi wa mazingira na itaambatana na Mjumbe wa Nyumba kumi au Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa na Afisa Mtendaji wa mtaa au wote kwa pamoja.

Timu hii itafuatilia mambo yafuatatyo:

(a) kuangalia kama usafi wa maeneo ya makazi, umma na shughuli za kiuchumi umefanyika;
(b) kubainisha na kuainisha mtu, kaya, kampuni, au taasisi ambayo haikufanya usafi na sababu za kutofanya;
(c) kuangalia kama takataka zimeondolewa na kupelekwa mahali panapohusika au zimeteketezwa kwa utaratibu muafaka; na
(d) kupeleka taarifa ya kulipa faini kwa mtu, kaya, kampuni au taasisi ambayo haikufanya usafi na kuelekeza namna ya kulipa faini.

Taarifa za ufuatiliaji zitapelekwa kwenye Kamati ya utekelezaji wa usafi wa mazingira siku ya Jumamosi ya kila Mwisho wa Mwezi ambayo itaandaa taarifa yake na kuipeleka katika Kamati ya Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira ambayo nayo itawasilisha katika mamlaka yake ya juu.

Ukusanyaji wa taarifa/takwimu/tathmini utafanyika kwa kutumia fomu maalum ya ufuatiliaji ambayo ni ***Kiambatisho Na. 1***.

**6.3.2. Ngazi ya Kata**

Kazi hii itafanywa na Kamati ya Mazingira ya Kata. Kamati hii itaripoti kwa Kamati ya Mazingira ya Wilaya. Shughuli hii itafanyika mara moja kila baada ya miezi mitatu.

Ukusanyaji wa taarifa/takwimu/tathmini utafanyika kwa kutumia fomu maalum ya ufuatiliaji ambayo ni ***Kiambatisho Na. 1***.

**6.3.3 Ngazi ya Halmashauri ya Mji, Wilaya, Manispaa na Jiji**

Shughuli za ufuatiliaji zitafanywa na Kamati ya Mazingira ya Halmashauri ya Mji. Kamati hii itawasilisha taarifa yake kwa Kamati ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya. Kamati ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya itawasilisha taarifa yake kwa Kamati ya Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ama Jiji kulingana na muundo na hadhi yake. Kamati ya Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa/Jiji itawasilisha taarifa yake Ofisi ya Makamu wa Rais. Kazi kubwa ya kamati hizi ni:-

(a) kufuatilia kama Tamko la Serikali la Siku ya Usafi wa Mazingira Siku ya Jumamosi kila mwisho wa mwezi linatekelezwa kama lilivyokusudiwa katika ngazi zote; na
(b) kubainisha upungufu uliojitokeza, kutoa ushauri ili kurekebisha ama kuboresha pale inapobidi na kuchukua hatua zinazostahili.

**7. ADHABU KWA AMBAYE HATAFANYA USAFI**

Taratibu za usafi wa mazingira kwa kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi zitasimamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na kanuni zake, Sheria za Sekta mbalimbali zinazohusiana na usafi wa Mazingira pamoja na Sheria Ndogo (By-laws) katika maeneo husika. Kanuni za Usimamizi wa Taka Ngumu za mwaka 2009 zitatumika kutoa adhabu kwa taasisi au mtu yeyote ambaye hataweza kusafisha mazingira ya makazi yake, ofisi au eneo lolote litakaloamuliwa kufanyiwa usafi.

***Kiambatisho Na. 1***

**FOMU YA UFUATILIAJI WA USAFI WA MAZINGIRA SIKU YA JUMAMOSI YA KILA MWISHO WA MWEZI**

***(Ijazwe na Kamati ya Usafi wa Mazingira kila Siku ya Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi)***

**Orodha ya uhakiki wa usafi wa mazingira katika Mtaa/Kitongoji cha…………………… Kijiji cha………………Kata ya………………………..... Jimbo la ........................................ Wilaya ya ......................................... Mkoa wa .................................**

**Tarehe ya usafi ......................................... Tarehe ya uhakiki…………………………………**
**(siku/mwezi/mwaka)**

**Eneo ambalo halikufanyiwa usafi na mhusika**

| S/N | MHUSIKA/JINA | ENEO/AINA | SABABU YA KUTOFANYIWA USAFI | MTAA/KITONJOJI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**JINA, WADHIFA NA SAINI YA MHAKIKI**

1.
2
3
4
5
6
7
8
9

NB: Fomu hii lazima isainiwe na Timu ya Ufuatiliaji na watu iliyoambatana nao.

Dar es Salaam,
13th April, 2016

JANUARY Y. MAKAMBA,
*Minister of State, Office of the Vice President,Union Affairs and Environment*